TANGAZO LA SERIKALI NA. 541 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI KOROGWE HILL YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Korogwe Hill ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ya mataji wazi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Korogwe Hill.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA KOROGWE


MSITU WA HIFADHI KOROGWE HILL

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 146 au Kilometa za Mraba 1.46

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Korogwe Hill linalopatikana Wilaya ya Korogwe, Mkoa wa Tanga kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2185 ya mwaka 1999 (Skeli 1:5,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 541(Linaendelea )*




| | |
|---|---|
| Dodoma, | ANGELLAH JASMINE KAIRUKI |
| ___24 Mei, 2024 | *Waziri wa Maliasili na Utalii* |